ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1. Mhe. Ali Abdalla Ali	Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini.
2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni.
3. Mhe. Mgeni Hassan Juma	Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake.
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais.
5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani.
6. Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais.
7. Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/Jimbo la Tumbatu.
8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais.
9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais.
10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
11. Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.
12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa na Rais.
13.Mhe. Juma Duni Haji Kuteuliwa na Rais.	MBM/Waziri wa Afya/
14.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais.
15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni.
16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge.
17.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe.
18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni.
19.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando.

20.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi.
21.Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni.
22.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole.
24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka.
25. Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake.
26.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/ Kuteuliwa na Rais.
27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake.
28.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi.
29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni.
30.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae.
31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake.
32.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu.
33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
34.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
35.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
36.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais
37.Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
40.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake

43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
44.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
45.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
46.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
47.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
48.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
49.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
53.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
54.Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Jimbo la Kiembesamaki
55.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
56.Mhe. Marina Joel Thomas	Kuteuliwa na Rais
57.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando)	Jimbo la Mkwajuni
58.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma	Jimbo la Bumbwini
59.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
60.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini
61.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi	Jimbo la Chambani
62.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
63.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
65.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
66.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
67.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
68.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
69.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
70.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi

71.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
72.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
75.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
76.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
77.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake
Ndugu Yahya Khamis Hamad	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Thalathini na Mbili - Tarehe 27 Juni, 2014

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) Alisoma dua

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 - Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati

(*Majadiliano yanaendelea*)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe ninayo taarifa kwamba hatua ambayo tumefikia kwenye hoja hii ni kumwita Mhe. Waziri ili atoe hoja juu ya hotuba yake hii ya Makadirio ya Mapato na Matumizi na Wajumbe waamue, Wajumbe wenyewe kwa bahati mbaya wa kuamua hawapo. Kwa hiyo, shughuli hii itakuwa si muafaka kuendelea kwa sasa, Wajumbe ninaowaona haraka haraka wanafika kiasi 15 na mimi nitakuwa wa 16. Taratibu zinatutaka tuwe Wajumbe angalau 41; nusu ya Wajumbe 82 wa Baraza hili kwa mujibu wa muundo wa Katiba kwa chombo hiki.

Sasa taratibu zinatutaka kwamba mpaka tuwe na Wajumbe hao ndipo tuanze kufanya maamuzi. Chombo hiki ndio kioo chetu na kioo sasa hivi kimeingia kiza kiasi hiki. Kwa hiyo, itabidi tuakhirishe kikao kwa muda, tena muda wenyewe hauwezi ukawa wa dakika tano au kumi, naelewa nyinyi mliopo mmekuja haraka sana ili kumaliza shughuli hii na pengine wengine hata hatukuwahi kunywa chai, ingekuwa kuna chai ya Spika leo ni siku nzuri mliopo mkanywe chai ya Spika, lakini haipo bahati mbaya.

Basi tukiakhirishe kikao, juhudi zinafanyika za kupiga kengele kama taratibu zinavyosema, lakini juhudi pia zifanyike ili angalau kuwapigia simu wale ambao pengine wako karibu.

Hali hii kwa kweli sio nzuri, haifurahishi, ni matatizo. Tuakhirishe kikao hiki hadi saa tatu na nusu (3:30) tuone hali itakwendaje katika juhudi ya kuwatafuta Wajumbe wengine.

Tena niwaombe sisi tuliopo natumai hatutafanya ile kazi ambayo kuna mdudu mmoja yeye hukusanya wengine na yeye hutoka. Sasa tusifanye kazi hiyo sisi tuliopo, tuwepo *around* hapa hapa ili ikifika saa tatu na nusu dakika chache kabla ya wakati huo tujumuike na hao wengine ambao watakuwa wameitwa ili tuje tuendelee na shughuli yetu.

Kikao nakiakhirisha kwa sababu ya ukosefu wa *quorum*, watendaji watawaita Waheshimiwa Wajumbe ili tuje kumaliza shughuli hii.

(Saa 3:06 asubuhi Baraza liliakhirishwa hadi saa 3:30 asubuhi)

(Saa 3:30 asubuhi Baraza lilirudia)

Mhe. Spika: Ehe Katibu una Wajumbe wangapi, hebu hesabu.

Katibu: Wajumbe 25.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe natoa taarifa kwamba tuko Wajumbe 25 ukichanganya na anayeongoza kikao hiki tuko 26, bado *quorum* yetu haijatimia.

Ingekuwa kuna mjadala unaoendelea kwa kuchangia basi angalau tungesogeza sogeza tukajaribu kuwaita wengine, lakini mwelekeo haupo. Kutokana na hali hiyo na kwa kuwa leo ni Ijumaa, mimi nadhani tukubaliane moja kwa moja kwamba kikao hiki kwa asubuhi hii kimeshindikana kwa sababu ya ukosefu wa akidi inayotakiwa iwepo, ili

kuendesha shughuli hizi. Kutokana na hali hiyo basi, kwa uwezo niliopewa kama Kiongozi wa chombo hiki sasa naakhirisha kikao hiki hadi saa 11 jioni leo.

(Saa 3:32 Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

Hoja za Serikali

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 - Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, ugonjwa wetu ni kuhudhuria vikao vya Baraza, huu ndio ugonjwa tulionao. Sasa Katibu hebu hesabu Wajumbe tulionao ni wangapi.

Waheshimiwa Wajumbe, Wajumbe waliopo sasa ni 30, haijafikia akidi inayotakiwa kupitisha shughuli zetu. Inatakiwa angalau tuwe Wajumbe 41. Hiyo ndio hali tuliyonayo. Nashukuru na Mnadhimu anaingia Mjumbe muhimu sana, lakini bado tunahitaji Wajumbe wapatao 10. Kiutaratibu hatuwezi tukafanya maamuzi, itabidi tukubaliane kwamba tutoke humu ndani tutafute Wajumbe wengine walipo. Ila tu inasikitisha kwamba hiyo ndio hali yetu mbele ya macho ya wananchi. Katibu chukua hesabu tena.

Naashiriwa kuna Wajumbe wanaingia pale, kwa hivyo tusitoke kwanza. Mjumbe mwengine ameingia, na Wajumbe wengine bado wanaingia. Na mwengine anaingia. Haya Katibu lete hesabu. Na mwengine anaingia sasa. Haya Katibu!

Waheshimiwa Wajumbe, idadi ya Wajumbe waliopo ni 42 na tuchukue ukiasi kwa hilo ingawa bado halijaridhisha. Isipokuwa niwaombe tu Waheshimiwa Wajumbe, kwamba hebu tujitahidi pamoja na machofu tuliyonayo tubakie humu ndani, kwa sababu wakitoka wawili tayari shughuli zetu zitakuwa zinakwama. Tujitahidi tuifanye kazi hii na wakati huo huo watendaji hasa Katibu namuomba aite wengine ambao bado wapo nje ili waje tushirikiane katika kazi hii. Katibu soma tena.

Hoja za Serikali

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 - Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati

(Majadiliano yanaendelea)

Utaratibu

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, kifungu cha 6 (g) kuhusu Kanuni haitokubali isipokuwa tu kama ifuatavyo:-

Hoja yangu, kuhusu hoja tuliyokuwa nayo Wizara hii ni nyeti, hoja baada ya kuwa tatu angalau zifike tano. Kwa kifungu cha 98 (3) "Endapo hoja ya kupunguza fungu kwa kupunguza kifungu chake fulani kidogo cha fungu hilo imekubaliwa au kukataliwa, hoja nyengine si zaidi ya mbili zinaweza kuruhusiwa juu ya kupunguza kifungu hicho".

Mhe. Spika: Mhe. Jaku Hashim Ayoub hebu soma kanuni inayosimamia hiyo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: 98.

Mhe. Spika: 98.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Naam, kifungu 3.

Mhe. Spika: Kwa hiyo?

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Hoja badala ya kuwa tatu kutokana na Wizara yenyewe kuwa muhimu kwa wananchi angalau ziwe tano au sita kama ulivyokuwa utaratibu wetu hapo nyuma.

Mhe. Spika: Unakusudia wakati wa kupitisha vifungu hapo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ndio.

Mhe. Spika: Basi hiyo hoja yako haijafika wakati.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante, ni kutoa taarifa mapema tu.

Mhe. Spika: Naomba sasa nimkaribishe Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kwanza naomba uwaruhusu watendaji wa Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati wateremke chini kwa idhini yako.

Mhe. Spika: Natoa ruhusa.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, baada ya kufanya majumuisho niliyoyafanya, naomba sasa kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya makadirio haya ya mapato na matumizi kwa Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati wanyanyue mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kwa kuwa Baraza limejadili na kuikubali Hotuba ya Bajeti ya Wizara yangu, sasa naomba Baraza lako Tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili kuvipitisha vifungu vya matumizi ya Wizara yangu.

Kamati ya Matumizi

Fungu 25	**-**	**Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati**	
Kifungu 0301	-	Ofisi Kuu Pemba	233,600,000
Kifungu 0501	-	Idara ya Ujenzi	11,300,000
Kifungu 0701	-	Hifadhi ya Mji Mkongwe	3,000,000
Kifungu 0901	-	Idara ya Ardhi na Usajili	3,510,000,000
Kifungu 1001	-	Idara ya Upimaji na Ramani	85,000,000
Kifungu 1101	-	Idara ya Nyumba na Makaazi	524,000,000
Kifungu 1401	-	Msajili wa Ardhi	30,000,000
Jumla ya Fungu			**4,416,900,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Fungu 25 - Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati

Kifungu 0301 - Ofisi Kuu Pemba

Kifungu 0401 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia nikitaka maelezo kuhusu nyumba ya *train* maarufu Darajani, maelezo yake na Waziri alinijibu vizuri sana na *Hansard* yake ninayo. Nilitaka kujua nyumba ile kapewa nani na usimamizi wa nyumba ile utakuwa wa nani na wale wenye maduka pale watasimamiwa na nani.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, ninapenda kujibu kama ifuatavyo. Nyumba ya *train* hajapewa mtu yeyote. Nyumba ya *train* inasimamia na Mamlaka ya Mji Mkongwe, wameiangalia, wameiona inahatarisha maisha ya watu wanaoishi mule. Kwa sababu hiyo, wameleta hoja Serikalini. Serikali imekubali kwamba nyumba ile ifanyiwe matengenezo makubwa ili kuwahifadhi wale na matatizo ya kuja kutokea hapo baadae. (*Makofi*)

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, Waziri ananijibu kwamba nyumba ile itasimamiwa na Mamlaka ya Mji Mkongwe. Lakini Mamlaka ya Mji Mkongwe ninavyojua mimi kuna kitengo kinachosimamia nyumba, sasa kama Mamlaka ya Mji Mkongwe imeshapewa *power* hii, kuna kitengo cha udhibiti wa nyumba pale Mamlaka ya Mji Mkongwe. Sasa ndio inahusika na huyu mkurugenzi mmoja au au vipi. Maana yake ninataka kujua kama inahusika na Mamlaka ya Mji Mkongwe, kuna idara mbili pale; kuna udhibiti wa nyumba na Mamlaka ya Mji Mkongwe. Sasa nilikuwa ninataka waziri anifahamishe anayesimamia jengo lile ni Mji Mkongwe au Idara ya Nyumba.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, nyumba za Mji Mkongwe zinasimamiwa na Mji Mkongwe wakati zinapokuwa zinatakiwa kufanyiwa matengenezo kwa ajili ya kuthibitisha kwamba inavyotengenezwa ndivyo.

Mjenzi anaweza kuwa si mtu wa Mji Mkongwe, anaweza pengine Idara inayodhibiti nyumba ikapewa hilo agizo, akatafuta *contractor* wa kuijenga ile nyumba au Idara ya Ujenzi wenyewe ikachukua dhamana ya kuijenga ile nyumba. Hiyo inaweza ikategemea hali itakavyokuwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, ninavyofahamu mimi kutokana na hali yetu ilivyo sasa hivi, kimapato Serikali, hali ni nzito sana na hairidhishi. Ujenzi wa pale tusitake kutiana mchanga wa macho, si wa leo wala kesho.

Hivi sasa Mahakama ya Ardhi ninafikiri wakati wowote dari yake itakuja chini, kuna nyumba juzi Chake Chake imeshaanguka kwa kutegemea pale Mhe. Waziri, sijui kama taarifa hizo unazo. Lakini kwa pale kujenga ujenzi ule, si wa leo wala si wa kesho.

Ulizungumza hoja katika maelezo yako ulivyokuwa ukijibu. Kwa mfano hata ukinunua *flat* katika *Chawl Building* utaitengeneza pekee yako hii ni tatizo, huwezi kutengeneza *flat* peke yako shirikiana na Serikali. Je, swali langu Mhe.Waziri. Upo tayari mimi mmoja muathirika katika jengo lile upo tayari nishirikiana mimi na wewe kuhusu jengo lile. Kwa kutegemea Serikali, si leo wala si kesho.

Hoja yangu ni kwamba upo tayari na si aibu kuingia ubia na mtu.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, nadhani anachokizungumza Mhe. Mjumbe ni kuwa na *partner* katika kulijenga jengo lile kama sitokuwa sikukosea. Sasa kama *partner* yupo ni vizuri ajichomoze, aje wazungumze na idara inayohusika, baadae waekeane masharti. Masharti yakiwa mazuri na wakiyakubali yote, wanaweza wakayafanya matengenezo ya nyumba ile kwa kutumia *partner*, hakuna matatizo yoyote.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nitakuwa sijamfanyia haki Mhe.Waziri, kama sikumshukuru kwa umakini wake wa kujibu hoja. Hii imenithibitishia mwaka jana na mwaka huu hata buti naona zitapungua kutokana na umakini wake na wizara kuonesha kuwa anaimudu uzuri.

Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana Mhe. Waziri, hongera sana. Mhe. Mwenyekiti, tuendelee. (*Makofi*)

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Mwenyekiti, ahsante. Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia nilizungumzia suala la hawa ndugu zetu wa *HUAWEI* katika suala zima zima la umeme. Mhe. Waziri, alipokuwa akijibu hoja ninahisi alisahau kutusaidia kutujibu suala hilo.

Naomba Mhe. Waziri, atupe ufafanuzi juu ya suala la hawa *HUAWEI*.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, *HUAWEI* anaweza akaweza, ni muekezaji hapa Zanzibar kwa kusaidia kuleta umeme au kuongeza kama ni chanzo mbadala cha umeme. Kitu muhimu kwa *HUAWEI* aombe kama walivyoomba waliotangulia. *Senricona* ameomba zamani, amewasiliana na *ZECO* mpaka wamekubaliana, wamepeana masharti ambayo *Senricona* anakwenda kukamilisha masharti sasa hivi kwa ajili ya kuleta ambavyo imeshaelekea kwamba watakubaliana. *HUAWEI* kama anataka kuzalisha umeme Zanzibar, mlango upo wazi, alete maombi yake na tukae pamoja tuone kwamba masharti yatakuwa muafaka bila shaka atapokelewa na yupo mwengine kama yupo zaidi ya *HUAWEI* anataka kuja vile vile, naye aje na kuleta masharti yake. Tunataka umeme wa jua, tunataka umeme wa mawimbi ya bahari, tunataka umeme wa upepo, tunataka umeme wa taka taka. Tunataka umeme wowote ambao utatusaidia hapa Zanzibar. (*Makofi*)

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana nimeridhika na majibu ya Mhe. Waziri na ninampongeza sana kwa majibu ambayo ameyatoa na awe tayari kupokea maombi kutoka *HUAWEI* kwa ajili ya kupatikana kwa umeme wa jua ndani ya visiwa vya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, ahsante tuendelee.(*Makofi*)

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Mwenyekiti, ahsante. Wakati nilipokuwa ninachangia nilizungumzia kuhusiana na nyumba ya maendeleo ya Kengeja. Nyumba ile nilisema kuwa ipo katika hali mbaya na wakati wowote inaweza kuleta maafa katika nyumba ile.

Nilimuomba Mhe. Waziri, atueleze majibu ya kina kuhusiana na mipango ambayo ameifanya ili kwenda kuifanyia ukarabati nyumba ile. Hivyo, nimuombe Mhe. Waziri, anieleze ni mipango gani ambayo ameifanya katika kuhakikisha kwamba nyumba ile inafanyiwa matengenezo.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba katika bajeti ya mwaka jana tulifanya *estimate* kwa ajili ya nyumba ile na katika buku la makadirio, tulitengewa shilingi milion mia mbili. Tukazifuatilia ili tuzipate tuanze kulifanyia matengenezo jengo lile. Bahati mbaya hatukupata hata senti moja katika hizo shilingi milioni mia mbili na tulizidai mpaka dakika ya mwisho hatukuzipata. Lakini hata hivyo, inaelekea kwamba hivi sasa hatukupewa pesa kwa ajili ya nyumba ya Kengeja, isipokuwa tunachojua ni kwamba upo utaratibu ambao utafanywa na Wizara ya Fedha kutafuta pesa mahali popote ili jengo lile lifanyiwe matengenezo.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Mwenyekiti, mbali na majibu ya Mhe. Waziri, lakini ningelimuomba Mhe. Waziri, kwamba kama nilivyozungumza wakati ninachangia tukashirikiana kwa kuweza kufanya ziara, kwenda kuitembelea nyumba ile ili aione hali ilivyo jinsi hali ya hatari ilivyo katika nyumba ile. Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri, basi tushirikiane kwa pamoja twende tukaitembelee nyumba ile ili aione. Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo naomba tuendelee.

Kifungu 0401 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti - Shs.181,339,000.00
Kifungu 0402-

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa ninachangia nilizungumzia hali mbaya ya miundombinu ya maji katika Jimbo la Rahaleo, ikiwemo maeneo ya Gulioni, Mlandege na Rahaleo yenyewe pamoja na Mwembeshauri na Miembeni.

Mhe. Mwenyekiti, Serikali au wizara husika imefanya bidii kubwa katika kupunguza tatizo la maji mjini. Lakini bado katika maeneo hayo niliyoyataja, tatizo lipo katika miundombinu. Ningemuomba Mhe. Waziri, ana mikakati gani katika kuhakikisha kwamba inafanya miundombinu ili kuondoa tatizo la maji kwenye maeneo hayo.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, tatizo la maji katika mji wa ng'ambu linaeleweka na kwa sababu hiyo, ndio *ZAWA* wakawa wanajitahidi kutafuta chanzo chengine cha maji zaidi ya kile kiliopo Mto Pepo na Mwanyanya. Kwa sababu Mto Pepo sasa hivi unaweza kusema ni karibu na ziro maji yanayoweza kupatikana pale na Mwanyanya maji yamepungua sana.

Kwa hivyo, ikabidi lazima watafute mahali pengine wachimbe visima ili waweze kuyateremsha maji Saateni kwa ajili ya kuweza kusambaza katika maeneo ya ng'ambu. Wameshachimba visima vitatu tayari na tayari vinatumika kwa ajili ya kutoa maji kwa ajili ya kuleta ng'ambu na ndio maana sasa hivi sehemu za Makadara tatizo la maji limepungua na pia tuna mradi mwengine pale wa visima viwili vya Ras el Khaimah ambavyo tayari vimeshachimbwa na vimeshajaribiwa na vina maji ya kutosha.

Hivi sasa ukenda Chumbuni pale utakuta Ras el Khaimah wanajenga tangi kwa ajili ya kuteremsha kuingia katika mtandao wa ng'ambu. Tunategemea kwamba visima vile viwili vya Ras el Khaimah vikianza kufanyakazi na vile visima vitatu, wakijumlisha pamoja nguvu zao maji yatapatikana ya kutosha pale Saateni na mtandao wa ng'ambu utapata maji ya kutosha.

Tunaendelea na hiyo kazi kwenye hatua nzuri. Namuomba Mhe. Mwakilishi, atembelee pale Chumbuni atakuta kwamba Ras el Khaimah hivi sasa wanamaliza kulijenga lile tangi na visima vipo tayari na watateremsha *pump* katika visima vile na litajazwa tangi lile linaloteremsha kupeleka kwenye maeneo ya ng'ambu.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mhe. Waziri, lakini bado jibu langu kutokana na miundombinu ambayo mabomba ya kuingiza maji kwenye maeneo yale.

Sasa nilitaka kujua wana mipango gani ili kuweza kufanya miundombinu maji kwenye maeneo hayo niliyoyataja wananchi waweze kupata, hata kama maji yatakuwa yapo mengi, lakini kutokana na miundombinu iliopo, kuna mabomba mengine yamepasuka, mengine yameziba. Sasa sijui kuna mikakati gani kuhakikisha kwamba kunafanywa miundombinu ili wananchi waweze kupata maji katika maeneo hayo.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi, kama ifuatavyo.

Hiyo hali *ZAWA* wanaijua na kwa sababu hiyo wale ni shirika na wanaruhusiwa kukopa, wameanza utaratibu wa kuwaomba watengenezaji mabomba wawakopeshe mabomba ili waweze kufanikisha hiyo miundombinu inayopita kumwaga maji katika maeneo yale ya ng'ambu. Hilo suala wameshalianza katika uanzishwaji mbali mbali wa mabomba ili wapate yale mabomba waweze kusambaza maji.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa majibu yake. *Inshaallah* tuendelee.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. Nilipokuwa nikichangia wizara hii nilitoa masikitiko yangu makubwa kuhusu Jimbo la Muyuni. Nilitoa mifereji Jambiani ya nje kwa gharama zangu kama ni Mwakilishi wala sio Serikali.

Ni sababu gani nilitaka kujua mifereji ile ikang'olewa na ikachukuliwa na imekwenda wapi? Haikutia Serikali mifereji ile, si mara ya kwanza wala mara ya pili, mifereji ile ikang'olewa waliokuwa wakitumia wananchi.

Hoja yangu tu ni kwamba Mhe. Waziri, aniweke sawa mkurugenzi amekwisha kunifahamisha na nimeshafahamu. Lakini wananchi kule itakuwa hawatopata kufahamu na chombo chao ndio hichi wananchi. Anihakikishie tu kwa ile mifereji tu haitokuja kung'olewa tena ikishakutiwa, ikishakuwa na msimamizi. Ni hilo tu Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Mhe. Mjumbe, amezungumza na *ZAWA* na *ZAWA* wamemfahamisha watakachokifanya pale Jambiani. Naomba wananchi wa Jambiani wasiwe na wasi wasi. *ZAWA* wana hesabu zao na wanajua panahitajika mifereji mingapi, watasimamia suala hilo na mifereji ya kurejeshwa itarejeshwa. Bila shaka ile itakayozidi itakuwa haitorejeshwa kwa sababu kuna kiwango chake cha kutia mifereji katika maeneo, sio kila mahali patiwe mfereji namna kama hiyo.

Hivyo, Mhe. Mwakilishi, wananchi wa Jambiani wasiwe na wasi wasi kabisa, hiyo kazi itafanyika na maadam Mheshimiwa amechukua juhudi na mimi ninamjua Mheshimiwa anazungumza sana na Mkurugenzi wa *ZAWA* na wanafika mahali wanaelewana katika matatizo ya maeneo mbali mbali ambayo yanakuwa yana matatizo ya maji. Kwa hivyo, ninapenda kuwatoa wasi wasi watu wa Jambiani wategemee kwamba hiyo kazi itafanywa, tena kwa mafanikio makubwa sana.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, ninataka kumuhakikishia Mhe. Waziri, tu, wala asihangaike kurejesha, nimesharejesha mimi mwenyewe tayari na tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, kuna maelezo zaidi.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, hakuna.

Kifungu 0402 Mamlaka ya Maji Zanzibar	-	Shs.2,300,000.00
Kifungu 0501 Idara ya Ujenzi	-	Shs.551,545,004.00
Kifungu 0701 Hifadhi ya Mji Mkongwe	-	

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, hapa nilikuwa na hoja tatu ndio ile nikasema tuweke Kanuni kando, ndio hapa kwenye Mamlaka ya Mji Mkongwe:

Hoja ya kwanza, nilikaribia kutaka kulia nikasema kitu cha mwanzo humu nije nioneshwe kibali cha Hospitali ya Mnazi Mmoja kuhusu eneo la kukalia wagonjwa. Nilikuwa mkaidi na nitaendelea kuwa mkaidi ili nihakikishe kabisa.

Nilisema nije nioneshwe kibali, niikamata Wizara ya Afya. Wizara ya Afya ikasema wao hawahusiki na mambo ya ujenzi. Kibali kinatoka Mamlaka ya Mji Mkongwe. Kwa kweli wananchi wetu wa pale wanaotoka Unguja na Pemba, wanapata shida kufika pale, wanapigwa na mvua na pahali pa kujificha mvua hamna.

Sehemu iliyokuwepo pale Wizara ya Afya imehifadhi ma-*files*, siwalaumu Mji Mkongwe, sijui kwa udogo wa Hospitali, palikuwa na sehemu ambayo wakoloni wamejenga kutoka muda ule kujificha mvua. Lakini pameekwa ma-*files* kwa muda huu. Kwa hivyo, nitahitaji maelezo kile kibali nioneshwe ili nikiachie fungu.

Hoja yangu ya pili, chombo hichi kimepiga marufuku kuhusu kuongezeka kwa kasi katika mahoteli pale Mji Mkongwe. Niliuliza tena hapa katika kipindi kile, yale marufuku imekuwa basi.

Hoja ya tatu, kila mwaka ninasimamia njia ya Forodhani Mhe. Mwenyekiti. Ile njia hakuna sababu ya kufungwa bado na leo *Hansard* nimetafuta ipo aliyojibu Mhe. Waziri, kuwa ile njia hakuna msingi wa kufunwa, ilifungwa njia kutoka Malindi hadi Forodhani mpaka penye wizara yako na njia ya Posta. Walipoona kuna matatizo kutoka pale *NBC* ikafunguliwa kuelekea Posta. Kwa nini kule kusifunguliwe.

Bado hatuwafanyii haki wananchi. Nitahitaji maelezo kwa sehemu zangu tatu hizo na hasa nitaisimamia kidhati kabisa hoja ya Hospitali ya Mnazi Mmoja wagonjwa kuteseka.

Mhe. Mwenyekiti: Kwanza hii kauli ya kuwa mkaidi, ukaidi si tabia nzuri, yaani kuwa mkaidi si tabia nzuri, kuwa mkorofi pia si tabia nzuri. Ni afadhali ungesema utakuwa mgumu kidogo, lakini kuwa mkaidi, ukaidi si tabia njema. Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, masuala ya Mhe. Mjumbe, yamehusu ujenzi wa mahali pa kuangalia wagonjwa pale Hospitali, imehusu njia ya Forodhani na yamehusu ujenzi wa

mahoteli katika Mji Mkongwe. Kwa hivyo, masuala yote yanahusu Mji Mkongwe kama alivyouliza na ndicho kifungu chenyewe tunachokizungumza.

Mhe. Mwenyekiti, nilifahamisha juzi hapa nilipokuwa nikijibu hoja pale kwamba *UNESCO* hawakutunga sheria kwa ajili ya Mji Mkongwe. Nilieleza wazi kabisa, sisi wenyewe tulipotaka kuutia Mji Mkongwe katika urithi wa Kimataifa, tulipoomba walitwambia tungeni sheria tuone kama kweli munataka huu mji muite katika urithi wa Kimataifa.

Sheria ikatungwa na sisi wenyewe Zanzibar. Ikaletwa kwenye Baraza hili la Wawakilishi, ikajadiliwa hapa na ikapitishwa hapa ndani ya Baraza hili la Wawakilishi. Baada ya kwisha kupitishwa sheria ikapelekwa *UNESCO*, wao wakaitizama wakaona sheria imekidhi haja ya kuufanya mji ule kwamba ni mji wa urithi wa Kimataifa. Hilo nilifahamisha vizuri.

Sasa kinachotuumiza sasa ni sheria yetu wenyewe. Mimi Waziri ninayesimamia sheria ile pamoja na Mamlaka ya Mji Mkongwe tunaosimamia sheria ile, lazima tuwajibike kwa mujibu wa sheria yetu ilivyoeleza katika kuutunza Mji Mkongwe.

Moja katika tatizo kubwa ni kuufanya kwa Mji Mkongwe kuwa na *traffic* kubwa. Mji Mkongwe unataka upunguzwe *traffic*. Kupunguza *traffic* tutapunguza kwa kuzuia baadhi ya njia. Ndio maana kuna baadhi ya njia zimezuiliwa kabisa.

Ujenge ujenzi unaofanana na hifadhi ya Mji Mkongwe. Ndio maana Mji Mkongwe unasimamia masuala hayo. Upunguze masuala ya mahoteli yasiwe mengi katika Mji Mkongwe, kwa sababu kusiwe na zogo, kwa sababu ni urithi wa Kimataifa, ninakubaliana na wewe hilo.

Katika suala la kupunguza njia, sio njia hii kubwa tu anayozungumza iliyofungwa mpaka zile ambazo zamani tulikuwa tukipenya penya nazo, pia zimefungwa sasa hivi haziwezi kuingia gari. Tunatekeleza sheria yetu. *UNESCO* wenyewe kila mara wanaleta muangalizi kutizama kwamba haya masharti tuliyoyaomba ambayo tulieleza katika sheria zetu tunayafuata. Ndio *UNESCO* wanachokifanya. Kwa hivyo, wanapotuita kule kwenda kutuhoji wanatuita na kutoeleza kwamba sheria yenu ilisema kwamba maafali ya Mji Mkongwe yatakuwa namna hii na hii, lakini mbona tunaona kuna kitu fulani kipya kimeongezeka tofauti na hiki.

Ni kweli tuna tatizo sasa hivi, kwa sababu Mji Mkongwe sasa hivi tuna hoteli 64, ni kosa kuwa na hoteli 64 mule katika Mji Mkongwe sasa hivi. Juzi wenzangu walikwenda katika mkutano kule *DOHA* na walielezwa kwamba masuala mengi mmeshayajibu, lakini bado kuna suala la hoteli 64, mbona nyingi na zinaendelea kupanda. Ndio nikasema kwamba ipo haja ya kufanya marekebisho ya sheria yetu. Tukifanya marekebisho tukatoka katika misingi ya hifadhi ya Mji Mkongwe, basi mji wetu utaondolewa katika hifadhi ya Kimataifa, tena tutafanya wenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, kama tumeamua kuingia katika hifadhi, ni vizuri tuendelee kubakia katika hifadhi, ukija kwenye suala la ujenzi wa nyumba ya kusubiria kwenda kutazama wagonjwa pale, kinachokawilisha ni maelewano juu ya suala hili la wakati Wizara ya Afya wanazungumza na Mji Mkongwe, ni kwamba watu wa Mji Mkongwe walisema mtakapojenga kitu hapa hamuwezi kutumia ma-*concrete* hapa na zege ni lazima mjenge kitu kinachofanana na hii bustani na wakakubaliana wakachora ramani, hii hapa Mhe. Spika, ninayo ramani inayoonesha bustani yenyewe ilivyo na waka-*propose* nyumba ya kujengwa pale ifanane na ile bustani Mhe. Mwenyekiti, nitampa mtu akuletee hapo ili uione ilivyokaa, hii hapa ambayo inachukua watu 400 kukaa pale kusubiri. Wizara ya Afya tayari wameshaikubali na wameshakubaliana hasa na Mji Mkongwe kwamba wajenge kitu kinachoweza kuhifadhi watu 400 ndani ya ramani hii.

Hii hapa mpelekee Mhe. Mwenyekiti, na hata kama kuna Mjumbe anataka kuiona mpelekee aione. Hiyo ndio jitihada ambayo tunaichukua, tumeshafika hapo sasa tumeshakubaliana na Wizara ya Afya wameshakubali kujenga kitu kama hicho na *pavement* ni kitu kizuri, watu 400 wataingi mule kusubiri kwenda kutazama wagonjwa ndani. Ni kitu cha kisasa kinafanana na bustani ilioko pale, hiyo ndio kazi inayofanywa na Mji Mkongwe.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, mpatieni hapo aone.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Iweke kwanza upande, kuna hoja nyengine. Ahsante Mhe. Mwenyekiti, hoja zangu zilikuwa tatu, nyengine zinaanza kuelekea. Lakini nije kuhusu njia ya Forodhani Mhe. Waziri, huku sisi wananchi wanatusikia na wanatuelewa chombo chao. Leo kama suala la *UNESCO*, mtu yuko Ulaya aje kutupangia sisi njia ya kuitumia barabara, hiki ni kitu cha ajabu. Kama *UNESCO* tumeona hoteli pale Mji Mkongwe, hoteli ya kileo na imepita hata juu, hii haiingii kichwani Mhe. Mwenyekiti. Nilisema sehemu hii nisiwe mkaidi, lakini nitakuwa mgumu kama nilivyosema.

Mhe. Mwenyekiti, leo mtu yuko Ulaya aje kutupangia chakula chetu hiki na hiki, mpita njia tu, kwa suala hili la *UNESCO*, hili haliingii kichwani. Kuna mahoteli yamejengwa juzi pale Mji Mkongwe. Leo wananchi kuitumia barabara wananiambia *UNESCO*. Mhe. Waziri hapa nitakuwa sikuelewi, leo barabara wananchi wasiitumie, hiki kitu hakifahamiki. Wakati waziri huyu hapa na kauli ipo hapa, utakaponiruhusu nitasema. Kuna waziri kasema ile njia mwisho nyumba ya kulelea watoto, sasa kauli zenu mawaziri zinagongana kwa wapi. Wale wananchi wamezaliwa hapa wasitumie barabara ile watatufahamu vipi wananchi.

Suala la pili, kuhusu hiyo ramani. Ndio tayari michoro hiyo tumeshaiona, lakini lini mtawakabidhi wenyewe Wizara ya Afya ili tupate kufuatilia ujenzi huo uendelee. Ni hayo mawili.

Suala la tatu, nafikiri keshasema marufuku Mji Mkongwe kuhusu majumba kuendelea na ujenzi, hilo nimeshalifahamu. Hoja zangu ni mbili tu na zaidi ni njia ya kutumia wananchi, hakuna msingi wa kufunga njia ile.

Mhe. Mwenyekiti: Nadhani Mhe. Mjumbe usingepandishia hoja, maana mwanzo kuhusiana na eneo la kusubiri watu kwenda kuangalia wagonjwa, ilikuwa ni hoja kama vile kibali kimetoka au laa. Kimsingi kibali kimetoka na ndio maana ramani ikachora. Sasa suala la lini hii, sijui labda waziri utusaidie.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, naweza nikaja kughafilika, kwa hivyo, niachie nilijibu vile nilivyolipata alivyolizungumza mwenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, nataka wananchi wafahamu hakuna mzungu aliyetupangia namna ya kuhifadhi Mji Mkongwe, ni sheria yetu wenyewe, ambapo kwa bahati nzuri baada ya Wajumbe kuipitisha imeingia katika vigezo vya uhifadhi wa Mji Mkongwe, moja wapo ilikuwa ni kupunguza kasi katika Mji Mkongwe. Hilo nataka wananchi waelewe hivyo kwamba hakuna mzungu kutoka *UNESCO* aliyekuja hapa akatupangia namna ya kuhifadhi Mji Mkongwe, tulitunga sheria sisi wenyewe na baada ya kuipeleka wakaitizama wakaona imekidhi haja. Sasa wanachokuja kukitizama ni kutizama tunaitekeleza ili iendane na urithi wa Kimataifa katika ule Mji Mkongwe.

Mhe. Mwenyekiti, suala hili nataka likae wazi kabisa. Sasa kama tunaona ile sheria inatubana sisi wenyewe, sheria ni yetu wenyewe, wale ni lazima watutizame. Wanapotuita wanatuambia, sheria yenu imeeleza kwamba mtafanya hili na hili mbona mnakiuka. Ndio *UNESCO* wanachokifanya na sio hapa tu, ni nchi zote zenye urithi wa Kimataifa wanatengeneza ile sheria.

Kwenye suala la kibali nimeshasema, kwanza walikuwa hawajaelewana tunachokizungumza baina ya Wizara ya Afya na Mji Mkongwe, wamefika hatua sasa wameshaelewana na wametoa *go ahead* juzi, leo ya tatu waandikiwe kibali siku mbili hizi wapelekewe. Sisi tunaikubali na tutajenga. Kwa hivyo, itabidi wapelekewe kibali hivi sasa, wao wameshakubali kila kitu na Mji Mkongwe umesharidhika na kitu kama kile kitajengwa na kitapendeza na pale mahali patapendeza. Kwa hivyo, hakuna mtu yeyote anayetupangia. Mhe. Mwenyekiti, ni sheria yetu wenyewe tuliotunga katika Baraza hili na lazima Mji Mkongwe waisimamie ile sheria na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi nao waisimamie hiyo sheria, maana wameitunga na kuipitisha wao.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru Mhe. Waziri na nimuombe sana kwa lugha nyepesi na laini sasa hivi na kuomba sio makosa. Mhe. Waziri, hebu nionee huruma mimi sasa, hii hoja inakuja kila mwaka mara tatu. Hii ni hoja nyepesi sana Mhe. Waziri, tuwasaidieni wananchi kutumia barabara yao. Maana yake pale bandarini *traffic* kubwa kuliko hii, kama ni *traffic*, basi Darajani kuna *traffic* kubwa kuliko ile Mhe. Waziri. Kwa hivyo, tuwaruhusu kile kipande sio kikubwa.

Mhe. Mwenyekiti, naomba uniruhusu nikisome;

"Serikali haikufunga barabara inayotoka Malindi na kuelekea Benki ya *NBC* Forodhani, ilichofanya Serikali ni kuzuwia vipando vya moto kupita mwisho wa jengo la Ngome Kongwe kuingia kwenye jumba lile pale chini".

Haya ni majibu ya Serikali sio yangu, mimi nikuomba tu, ni kipande kidogo sana kile turuhusu tuendelee tusipoteze muda, wewe ni mzee wangu Mhe. Ramadhani Abdalla Shaaban na majibu ya Serikali kama kauli za Serikali zinagongana, basi mimi sina la kusema tena. Hayo sijazungumza mimi ni *Hansard* ya swali nambari 6 ya mwaka 2011.

Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri, kile ni kipande kidogo tu tusipoteze muda tukabishana. Wewe ni mzee wangu waruhusu kile kipande wananchi wakitumie.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, kama Mwenyezi Mungu atatupa uwezo tutakapokwenda kwenye Mkutano wa *World Heritage*, ingekuwa vizuri nikamchukua na Mhe. Jaku Hashim Ayoub, siku moja, akaenda kuwaona *World Heritage* wanavyoisimamia sheria yetu ili kutona tunaitekeleza, basi angeona vizuri sana, kusema kweli, sheria ni yetu wenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, sasa kama kuna suala la kuibadilisha angoje na sisi tumeshasema tutaleta marekebisho hapa, siku hiyo atakuja kutoa mchango wake *Inshaallah* Mwenyezi Mungu akipenda kupunguza ile sheria kama itakubaliwa tena kule, lakini pia, itabidi tuwashauri tukiweka hivi, je, mtatukubalia. Wanaweza wakakataa wakasema mji wenu tutauweka *in dangerous*, maana hivi sasa wanataka kutuweka kwenye *in dangerous* kutokana na mambo mambo mbali mbali. Yeye analizungumzia suala la njia tu, kuna mengine mengi tu kama *traffic* kubwa sana, watu wengi sana unakuwa ule Mji Mkongwe unakaa mabaskeli na mambo mengi, hautaki vile. Hiyo ndio hali halisi.

Mhe. Mwenyekiti, sisi tunaitwa kule tunawekwa kiti moto kwa kutekeleza sheria yetu na sisi tunalinda Mji wa Zanzibar usitoke katika *World Heritage*, ni moja katika sifa ya Zanzibar kuwa tuna Mji Mkongwe wa asili na unatambulikana kama ni *World Heritage,* kama ilivyo ile bustani inayoning'inia kule *Baby lone* na kwengineko ndio tunaulinda uwe hivyo mji wetu.

Mhe. Mwenyekiti: Wacha tufanye hivi, kwamba jambo hili tusifanye maamuzi ndani ya chombo hiki hivi sasa, ni jambo ambalo linahitaji mazungumzo kati yetu sisi wenyewe na wasimamizi au wadhamini wa hiyo *World Heritage,* ili tuone baadhi ya mambo ambayo tunaitaji labda yawemo na yaendelee katika Mji Mkongwe, wazungumze wizara, wakazungumza na wenzetu waseme kama hili na hili mnaweza mkarekebisha na kama mtarekebisha maana yake sheria hiyo irekebishwe kama alivyosema Mhe. Waziri, lakini kuliamua hapa, basi matokeo yake tunaweza tukalaumiana baadaye. Ni suala la kukaa waka- *negotiate* kati ya wizara na wadhamini wa *World Heritage* kuhusiana na miji mbali mbali.

Kwa hivyo, nadhani tuwache kazi hiyo ifanyike ili tuone nini kinaweza kikarekebishwa katika sheria, lakini bado mji wetu ukawa uko katika urithi wa Kimataifa. Sasa Mhe. Jaku Hashim Ayoub, nikuombe kwamba hiyo hoja uiache ifanyiwe kazi na wizara inayohusika, hatuwezi tukaiamulia hapa. Jambo ambalo haliko kwetu moja kwa moja. Labda tukisema kwamba sasa basi uwepo chini ya urithi wa Kimataifa, tukisema hivyo kitu chengine, ni kiasi cha kui-*draw* ile sheria, basi tukafanya tunavyotaka na ndivyo anavyosema Mhe. Waziri. Kwa hivyo, kazi hii ifanywe na wizara wala tusiifanye ndani ya Baraza hili. Tusiwe watendaji, maelekezo ni hayo wizara ikae kitako na shughuli hiyo iendelee. Mhe. Jaku Hashim Ayoub, tuachie tuendelee.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kuhusu kufunga njia ile haihusiki *UNESCO* ni kutiwa mchanga wa macho, wala sio sheria kufunga njia ile, ni hilo tu. *UNESCO* haihusiani na njia ile, hiyo ni kutiwa mchanga wa macho, nina hakika mimi kwa suala hili na sio sheria kufunga njia ile.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim Ayoub, hilo suala tuliache, kwa sababu kupunguza *traffic* utafanyaje, ukisema unazuwia gari, maana yake ndio unapunguza *traffic*, lakini gari zitakwenda tu kama njia ziko wazi. Kwa hivyo, iwache kazi hii ifanyike kwa pamoja, wizara na mamlaka ya Mji Mkongwe ili wafikie pahali waone nini ambacho kinaweza kikasaidia ili mji ule uendelee kupendeza, mji ule uendelee kuwa chini ya urithi wa Kimataifa na wananchi wapate kuufaidi mji wao. Mimi nadhani utuachie kazi hiyo ifanyike.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, tatizo hili sasa ni miaka mitatu na hakuna kinachoendelea humu ndani, umekuwa ni wimbo wa Taifa na mbuzi kumpigia gitaa tu na hoja hii naisimamia mimi siku zote.

Mhe. Mwenyekiti: Hivi Mhe. Jaku Hashim Ayoub, tuamuwe nini hapa? Unataka tuamuwe njia ufunguliwe halafu tufutwe, hilo hatuwezi tukaamua hapa. Wacha kazi hiyo ifanywe na wizara. Tuendelee.

Kifungu 0701	Hifadhi ya Mji Mkongwe-	374,465,600
Kifungu 0801	-	

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, mimi sina nina ya kuzuwia fungu hili, lakini juzi ambapo nilikuwa nachangia nilizungumzia kuhusu nguzo mbovu ya umeme ambayo ilikatika Mwembe Shauri pale Msikitini, Jimbo la Rahaleo Shehia ya Mwembe Shauri.

Mhe. Mwenyekiti, juzi nilisema kwamba namshukuru sana Mhe. Rais wa uteuzi wake wa waziri huyu ambaye yupo tunaendelea naye katika wizara hii pamoja na Katibu Mkuu.

Mhe. Mwenyekiti, juzi baada ya kuchangia tu, basi jana nguzo ile imekwenda kubadilishwa na kuwekwa nguzo mpya. Kwa hivyo, nimetumwa na wananchi wa Jimbo la Rahaleo Shehia ya Mwembe Shauri kutoa shukrani zao baada ya kwenda kubadilishwa nguzo ile jana na kuweza kuondoa hofu ya wananchi katika shehia ile. Kwa hivyo, nimshukuru sana Mhe. Waziri, Katibu Mkuu pamoja na *Manager* wa *ZECO* kwa kazi nzuri ambayo wameifanya na niseme tu kwamba wananchi wanapopeleka matatizo yao katika shirika pamoja na viongozi wao sisi, basi watendaji waelewe tu tusingoje mpaka mengine tuyalete hapa Barazani ili yatekelezwe.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, ilikuwa ni shukrani tu unapewa katika hili. Mhe. Mahmoud Thabiti Kombo.

Mhe. Mahmoud Thabiti Kombo: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii, naomba nimpongeze sana Mhe. Waziri, kwa majibu yake mazuri, ufafanuzi anaoutoa kwa ufasaha ambao naamini wananchi wa Zanzibar wanaendelea kuelimika. Kwa malengo hayo hayo au kwa nia zetu sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, kila tukiomba ufafanuzi, basi ile faida inakuwa sio ndani ya ukumbi huu tu bali ni kwa nchi yetu nzima.

Mhe. Mwenyekiti, nimesimama hapa sina nia ya kuzuwia kifungu wala fedha yoyote ile. Ila nilikuwa naomba...

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, naona tunatoka na tunaendelea na kazi hii sijui tutafanyaje. Kama kuna dharura, basi iwe dharura ya mara moja turudi. Endelea Mhe. Mjumbe.

Mhe. Mahmoud Thabiti Kombo: Ahsante Mhe. Mwenyekiti. Mimi nimesimama hapa ili kuomba tu ufafanuzi, kwa sababu suala hili limekuwa likizungumziwa muda mrefu na kuna mikataba mbali mbali ambayo imesainiwa na viongozi wetu wa Kitaifa na Mhe. Waziri, mwenyewe juu ya masuala ya gesi na mafuta na sisi wanyonge hali zetu maskini. Mhe. Waziri wa Fedha, jana alikiri hapa tuna-*deficit* kama asilimia 40.

Kwa hivyo, nilikuwa naomba kupata ufafanuzi wa Mhe. Waziri, kwamba hayo mafuta na gesi asilia, hiyo mikataba imefikia wapi na lini tunatarajia kazi hiyo ya upembuzi ama *exploration* itaanza. Nashukuru.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Ahsante sana. Mhe. Mwenyekiti, gesi asilia na mafuta kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano lilikuwa ni suala la Jamhuri ya Muungano na mpaka hapa ninapozungumza bado ni suala la Jamhuri ya Muungano.

Mhe. Mwenyekiti, palikuwa na mikataba mingine ilikamilika, lakini haikupata kuendelea kwa sababu ya maombi yetu sisi Wazanzibari na mengine haikukamilika. Kuna eneo ambalo lilitolewa rasmi kwa ajili ya *ANTRIM*, walipewa hiyo *offer* na wakasaini *PSA* ili waendelee na utafutaji wa mafuta katika *zone* ya Unguja na Pemba, lakini hiyo ilikuwa ni *on shore,* sio *off shore.* Lakini ilikuwepo *offer* ambayo ilitoka kihalali kabisa ambao walipewa *shell*, lakini kwa bahati hawakuwahi kusaini *PSA*.

Mhe. Mwenyekiti, lakini baada ya sisi kupeleka maombi ya kusema kwamba sasa gesi na mafuta tuwachiwe sisi wenyewe Wazanzibari, kwa bahati *ANTRIM* alikuwa ameshauza mkataba wake kwa *RAK GAS*. Kwa hivyo, *RAK GAS* ikabidi sasa hawezi kuendelea na utafiti wowote ni lazima waje Zanzibar kuomba ruhusu ya kuendelea na hayo masuala ya *seismic shooting* na mambo mengineyo. *Shell* hakuweza kufanya hivyo, kwa sababu alikuwa bado hajasaini, na kwa sababu wote walipata taarifa sasa unakokwenda katika eneo la Zanzibar ina maana sasa hivi uende Zanzibar katika kufanya maombi. Sasa ndio maana tukawa tunazungumza hapa na *Ras Gas*, tukawa tunazungumza hapa na *Shell* tunazungumza vilevile na wengine wanaokuja kutaka kuomba kwenda kama *State Oil* na wengineo ambao wanakuja kuomba.

Katika Jamhuri ya Muungano tulifikia makubaliano kwamba *gas* na mafuta yaondoshwe katika katiba ya Jamhuri ya Muungano. Mhe. Mwenyekiti hivi sasa tuko Dodoma na ukiisoma ile rasimu *gas* na mafuta vimeshaondoshwa katika ile rasimu. Tukikamilisha kikao chetu mwezi wa Agosti huko, maana yake *gas* na mafuta ziko chini ya Zanzibar. Lakini hawa wote tumewazuia wasiendelee na kitu chochote hivi sasa na ndio maana hizo *blocks* zetu nne ambazo zilikuwa zimekaa bila ya kufanya kitu chochote na hii ya *On show* ambayo imekuwa *Ras Gas*, imekaa bila ya kufanya kitu chochote tunangojea tupitishe katiba, tujue kile kitu sasa hivi ni chetu wenyewe, sasa waje tufanye majadiliano nao upya kwa masuala haya, tukubaliane masharti.

Kwa hivyo kusema kweli hatujafikia kiwango cha kumwambia *Ras Gas* sasa fanya *shooting* utizame kiwango cha mafuta na kila kitu, hatujafika kiwango hicho. Wala *Shell* hatujawaambia hivyo kwa sababu *shell* hata *PAC* hajasaini. Hiyo ndio hali halisi tuliyofikia sasa hivi. Twendeni Dodoma tukazungumzeni katiba mwezi wa Agosti keshokutwa kupitisha katiba yetu tuje tufanye mambo yetu hapa.

Mhe. Mahmoud Thabit Kombo: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti na naomba nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa ufafanuzi wake.

Mhe. Mwenyekiti: Wajumbe mnaoondoka nakuombeni sana murudi ili tuendelee na kazi.

Mhe. Mahmoud Thabit Kombo: Nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa ufafanuzi wake na naamini Dodoma tutashirikiana nae bega kwa bega katika jambo hili, Ahsante sana.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti nilipokuwa nachangia nilisema kuna wananchi wangu wa kijiji cha Paje wamekusanyiwa shilingi elfu nane kwa ajili ya umeme wa mkopo, leo karibu inakaribia mwaka au nusu mwaka; muda mrefu zile pesa, wamezipeleka kule nafikiri ni za kukopeshwa ukalipa ziada wamewakamatia Shirika la umeme! Ni lini watawapelekea umeme ule kule Paje na sehemu ya Jambiani?

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti elfu nane ni pesa za fomu unapotaka kuomba mkopo unakabidhi shilingi elfu nane, unajaza ile fomu, fomu wameshajaza sasa sijui kwamba walitegemea kwamba waitwe, lakini nimezungumza na *ZECO* na wanasema sisi tunataka watu hawa waliokwisha kulipa Shilingi elfu nane waje tuwakamilishie utaratibu wa kuwapa mkopo, na wakiweza kufikia masharti yetu tutawapa mkopo. Kwa hivyo sio wa Paje tu hata wa sehemu nyengine ambao wamenunua fomu kwa ajili ya mkopo, waende *ZECO* kwa ajili ya kufanikisha suala la kupatiwa huo mkopo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mzee wangu miadi ya *ZECO* walikuwa kwenda kule kuangalia eneo na hajapita na wala hakuna harufu yoyote ya kuwa atakwenda kule hadi hii leo. Kwa mujibu wa wananchi wangu walivyonituma mimi muwakilishi wao baada ya kuchukua hizo pesa, hakuna hiyo harufu ya kwenda mpaka hivi leo alijue tu Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, mtu anapotoa pesa zake azifuatilie pesa zake ni haki yake. Nashukuru kwamba wamemtuma muwakilishi wao sasa kwa sababu hawajenda kutizama na ananieleza hapa kwamba hawajenda kupimiwa kule. Sasa ananiambia mimi Waziri niwaambie ZECO waende wakawapimie, naichukua hiyo kazi na watakwenda kuwatizama.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti naomba tuendelee lakini isijekuwa kama nguzo za Pete zilizoanguka mpaka leo miezi sita, tusije tukafikia hapo.

Kifungu 0801	Idara ya Nishati	277,935,400
Kifungu 0802	Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma	399,800,000
Kifungu 0901	Idara ya Ardhi na Usajili	264,051,600
Kifungu 1001	Idara ya Upimaji na Ramani	420,761,800
Kifungu 1101		

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nachangia nilizungumzia tatizo la nyumba hizi za maendeleo kuhusu mifereji ya maji safi. Mbali na majibu ya Mhe. Waziri lakini Mhe. Mwenyekiti leo nilifanya ziara katika jumba Na.3 na Na.4 Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli bado hilo tatizo lipo na tatizo kubwa katika jumba Na. 3 maji yale ambayo ni maji taka katika jumba lile, huwa yanatoka na yanapita barabarani na kupita pale *Quality Super Market,* kwa kweli inakuwa ni hali mbaya. Sasa nilizungumza hapa kwamba Idara ya Nyumba na Manispaa wanakuwa kama mpira wa kona hivi; kila mmoja anawaniya. mmoja anataka kufunga na mwengine anataka kuzuiya.

Sasa hapa kila mmoja Manispaa ukienda anakwambia ule si wetu, sasa nataka kujua msimamizi hasa wa matatizo yale ni nani? Kama ni Idara ya nyumba; muna mikakati gani ili kuliondoa tatizo lile? Kwa kweli hali siyo nzuri katika majumbe hayo ya maendeleo, sio jumba Na.3 tu na Na.4 lakini hata hayo majumba mengine ya maendeleo yakiwemo jumba Na.2 Na.1, Na8 yote Mhe. Mwenyekiti tatizo hili lipo. Kwa hivyo nilikuwa nataka maelezo ya kina kutoka kwa Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti analolizungumza Mhe. Mjumbe ni kweli na unapokuwa na nyumba suala la kuziba karo nalo ni suala la kawaida litatokeya ,unachotakiwa ni kwamba unafanya matengenezo wakati maharibiko yanapotokeya, ndio maana Idara ya Nyumba ukisoma kwanye bajeti yake wamezungumzia suala la kufanya matengenezo ya baadhi ya makaro katika Mji Mkongwe. Nakuhakikishia masuala haya ya maji machafu Unguja tunaita maji machafu sio maji taka. Wanafanya matengenezo katika kudhibiti haya maji machafu. Nashukuru kwamba Mheshimiwa ameleta hiyo taarifa na kwa sababu watu wa Idara ya Nyumba tunao na leo tunapitia bajeti na wamelenga vile vile safari hii kuhakikisha kwamba wanaendelea na kufanya matengenezo ya makaro ya maji machafu.

Kwa hivyo namuomba Mheshimiwa astahamili kidogo tuwape nafasi waende wakafanye haya matengenezo. Mimi sisemi kama suala la kutengeneza makaro ni kazi ya nani, najua mwenye nyumba aliyempangisha mtu ndio anatakiwa yakitokea maharibiko midam mtu analipa kodi atengeneze hiyo najua. Kwa hivyo najua Idara ya Nyumba inayo kazi hiyo, na nikisoma ripoti zake nakuta kwamba wanafanya kazi hiyo katika maeneo mbali mbali.

Mhe.Nassor Salim Ali: Mhe. Mwenyekiti nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mhe. Waziri, lakini kipindi tulichokuwa nacho kipindi cha mwezi wa Ramadhani na unajua tena unapofunga ukipita pahali ukakuta uchafu, pengine unaweza kufungua kwa harufu mbaya. Sasa nimuombe tu Mhe. Waziri kuhakikisha kwamba katika kipindi hiki basi yanakwenda kufanyiwa matengenezo, ili kuondoa tatizo hili baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Kifungu 1101	Idara ya Nyumba na Makaazi	239,898,800
Kifungu 1102	Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba	13,200,000
Kifungu 1201	Mahakama ya Ardhi	

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, nilisema kama kuna jengo lile la Mahakama ya Ardhi la Majestic hali yake hairidhishi na boriti zake hivi sasa nafikiri zimeshaanza kuvuja. Ningemuomba Mhe. Waziri akakaa akenda kuliangalia lile jengo na sijui lini watahamishwa kutokana na usalama wao mle ndani. Maana yake usalama hauridhishi wa jengo lile.

Hoja ya pili Mhe. Waziri alijibu vizuri sana lakini mpaka sisi tupige kelele wazee wa Mahakama ndio walipwe wale ma-*assessors* karibu miezi sita au nusu mwaka wanadai wale watu, ningemuomba tu pakawa na *formula* maalum badala ya kutegemea OC kuwa na *formula* Katibu Mkuu Wizara Fedha na Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi, kuwe na *formula* maalum hivi baada ya kwisha kulipwa, tutakuja tena mwakani tupige kelele tena. Hoja zangu zilikuwa mbili Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti nilipokuwa nikitoa ufafanuzi nilikiri kwamba hiyo kazi tunaifanya na nilisema kwamba tunawatafutia nyumba, ili wakakae katika nyumba ambayo iko salama zaidi kuliko ile ambayo wapo sasa hivi. Hilo nimekiri na hiyo kazi tunaifanya na hiyo nyumba hata tukiipata itabidi tufanye matengenezo. Wizara yangu iko tayari kuifanyia matengenezo nyumba hiyo, ili wahame na si Mahakama ya Ardhi peke yao wamo na wenzao mle bodi ya usajili, nao pia tunataka tuwatoe mle tuwatafutie mahala pazuri wakae, nilijibu hili wakati nilipokuwa nafanya majumuisho yangu.

Suala la ma-*assessors;* fedha walizolipwa juzi kama ingelikuwa idadi ya ma-*assessors* hawakuongezeka kutoka kile kiwango walichokitaja, fedha zile zingetosha kwa ajili ya muda wao wote ambao walikuwa wanadai. Lakini kwa sababu ma-*assessors* wameongezeka, hivi sasa kutoka wale wachache tuliokuwa nao nyuma imebidi sasa hivi pesa zetu tumewalipa wale na zimemalizika, na naahidi kwamba ndani ya miezi mitatu tutawamalizia deni lao lote, na watakuwa hawatudai. Tukija kwenye kikao hapa kijacho ni vizuri Mheshimiwa awafuate awaeleze na awaulize kama bado wanadai, ili tupate suala kwenye kikao kijacho tujue kwamba hatukutekeleza.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kidogo yanaelekea masuala kukaa sawa lakini bado, lini watahama lile jengo liko katika hali ya hatari Mheshimiwa aende akalikague. Suala la ma-*assessors* kama hatukuja kupiga kelele sisi wawakilishi litaendelea, mimi nimempa *formula* kama ataikubali au ushauri kama ataupokeya, waandae utaratibu wasitegemee pesa za OC. Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi watafute njia, wakae pamoja kuhusu suala hili. Hawa wakishafika miezi mitatu watatuma, sisi tu tufanye, kelele itakuwa miezi sita mingine, kwa hapo watafute *formula* maalum kwa kitengo hiki. Wale wazee hali zao taaban! Huu ni ushauri Mhe. Waziri kama umeukubali sawa, umeukataa basi.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, kama bado hujapata nyumba huwezi kusema lini utahama. Kwanza upate nyumba na nyumba hiyo utizame inahitaji matengenezo gani, tayari ni fungua mlango ingiya au kunataka matengenezo mawili matatu tuyafanyie. Kwa hivyo suala la kujibu lini watahama siwezi kulijibu hapa. Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tunazungumza suala tuwatoe wote wawili, sio tumtoe yule wa Mahakama wa Ardhi tumtoe pia na usajili wa ardhi nae pia atoke pale, tumpeleke mahala akakae, akafanye kazi kwa usalama. Kwa hivyo suala la kusema lini atahama itakuwa sina.

Hilo suala la kukubaliana na Katibu Mkuu nasema ni rai nzuri Waziri wa Fedha yupo amenisikia kama atakubaliana, hivyo hakuna tatizo. Lakini nataka nikufahamishe kwa nini sasa hivi tunaingia kwenye madeni haya, ni kwa sababu ya madai ya Wajumbe wa Baraza hili kwamba kesi za ardhi zinalimbikizana kila siku. Sasa hivi wanakutana kila siku wanakwenda badala ya zamani walikuwa wanakaa pale pengine wiki mara moja au wiki mbili mara moja, ndio maana hili deni limekuwa katika kiwango hiki. Lakini sasa hivi karibu kila siku na ndio maana kesi zinazosikilizwa nyingi na wanafika pahala wanatoa maamuzi, zile wanazotoa maamuzi. Kwa hivyo rai ameshaileta Serikali ishasikia, Wizara ya fedha ikikubali kutuwekea utaratibu huo mimi nitashukuru kwa sababu mimi sipendi kudaiwa kabisa. Kwa hivyo nitashukuru tukiondoa deni lao wale watu, itakuwa ni vizuri kabisa nakubaliana nae kabisa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mhe. Waziri. Ushauri kapokeya, sawa hauna tatizo. Suala bado hali ndio kama ile nyumba niliyokuuliza, suala la nyumba ya train, matokezeo yake ulisema ile nyumba hairidhishi inafanana na ile, usalama Mungu atujaalie lisije likatokea la kutokea. Mhe. Waziri afanye hatua za dharura kuishughulikia. Kama nilivyokwambia ikiwa Serikali itakuwa haina uwezo wa kujenga na sisi ndio waathirika katika lile jumba, ndio ukanambia uko tayari Serikali kushirikiana, ndio nikakwambia mimi nitaleta barua yangu ya mwanzo itakuwa kwa suala la jumba lile, lakini bado watu wanazidi kuteseka mle ndani. Mhe. Mwenyekiti tuendelee.

Kifungu 1201	Mahakama ya Ardhi	173,553,200
Kifungu 1301	Idar ya Uendeshaji na Utumishi	927,198,600
Kifungu 1401	Usajili wa Ardhi	183,772,000
Kifungu 1501	Idara ya Mipango Miji	278,233,000
Jumla y Fungu		**7,760,100,000**

(*Vijifungu vilivyosomwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu 0401	Idara ya Mipango Sera na Utafiti	23,283,090,000

Kifungu 0801	Idara ya Nishati	2,567,600,000
Kifungu 1001	Idara ya Upimaji na Ramani	948,168,000
	Jumla ya Fungu	**26,798,858,000**

(Vijifungu vilivyosomwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Baraza Lilirudia

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha makisio ya fedha ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati bila ya mabadiliko sasa natoa hoja kwamba Baraza liyakubali makadirio hayo.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe niwahoji, wale wanaokubaliana na makadirio hayo ya Wizara hii ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwka wa Fedha 2014/2015 – Wizara ya Fedha

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe mnaotoka nje naomba sana mbaki ili tuendelee na kazi hii.

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Spika, baada ya kutoa maelezo juu ya hoja walizozitoa Waheshimiwa Wajumbe, sasa naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Niwahoji Waheshimiwa Wajumbe, wale wanaokubaliana na hoja ya Makadirio ya Wizara ya Fedha wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Spika, kwa kuwa Baraza limejadili na kuikubali hotuba ya bajeti ya Wizara ya Fedha, sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi, ili kuvipitisha vifungu vya matumizi ya Wizara yangu kama vilivyo.

KAMATI YA MATUMIZI

FUNGU 19 - WIZARA YA FEDHA

Kifungu 0202	Idara ya Kodi za Ndani	55,502,958,000
Kifungu 0203	Idara ya Forodha	110,553,042,000
Kifungu 0401	Idara ya Mipango, Sera na Utafiti	5,015,000,000
Kifungu 0701	Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali	78,000,000,000

Kifungu 1301	Idara ya Uhakiki Mali na Mitaji ya Umma	992,500,000
Kifungu 1801	Bodi ya Mapato Tawi la Pemba	8,118,818,000
Kifungu 2203	Bodi ya Mapato Ofisi Kuu Zanzibar	173,214,082,000
	Jumla ya Fungu	**431,396,400,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

Kifungu 0301 Ofisi Kuu Pemba 1,146,119,000
Kifungu 0401 Idara ya Mipango Sera na Utafiti

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, mimi nilichangia kwa maandishi na alipokuwa Mhe. Waziri akajibu mimi sikuwepo lakini nilisoma *hansard* na nikaridhika sana na majibu ambayo alikuwa ameyatoa Mhe. Waziri. Nimesimama hapa Mhe. Mwenyekiti, kumpongeza tu Mhe. Waziri kwa kazi nzuri aliyoifanya hususan kwa mizigo ya wafanyabiashara ambayo ilikuwa ina matatizo. Amesimamia vizuri na mambo yamekwenda vizuri, ninashukuru sana na naomba utaratibu ule uendelee. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Mwenyekiti, ninashukuru sana, nimepokea shukurani nasema ahsante.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nachangia maana naona sasa ndio tunamalizia; nilizungumzia suala la kuiga bajeti kama ya wenzetu Bara. Nimesema hivyo kwa sababu tunalazimisha kitu ambacho tumeshakipitisha huko nyuma kwamba tunamtaka Waziri afanye hili na hili wakati bajeti tumeishapitisha kwenye Kamati. Sasa nimuombe Mhe. Waziri wakae, walitafakari maana jambo jema likiigwa sio baya, ili na sisi tuwaige wenzetu Bara wanavyofanya bajeti. Kwa sababu pale ndio unaweza ukaomba chochote kwa sababu hatujafanya chochote, ndio unaweza ukamuomba Mhe. Waziri au Wizara ya Fedha husika, kwamba tunataka Wizara hii iongezewe, kitu moja, mbili, tatu. Kwa hivyo ninamuomba sana Mhe. Waziri hilo alichukuwe, ili tuweze kwenda kwa mnasaba na wenzetu. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli wakati Mhe. Asha Bakari alipokuwa anatoa michango yake, alieleza swali hili na nataka nimuombe radhi kwamba sikuwahi kutoa ufafanuzi, lakini suala hili nalo serikali tayari imeshaikabidhi Wizara ya Fedha na tayari sasa hivi Wizara ya Fedha wataalam wetu wanaangalia *experience* ya wenzetu, na hawaangalii *experience* ya Tanzania Bara tu wanaangalia mpaka *experience* ya Uganda. Kwa sababu wao wana *model* tofauti, baadae ndio tunatakiwa tuje tutoe taarifa, ili tuseme *model* gani tuweze kwenda na baadae tutaleta utaratibu ndani ya Baraza lako tukufu.

Mhe. Asha BakariMakame: Tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu 0401 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, tulikubaliana na Mhe. Waziri wala nisizuie fungu, lakini nilikuwa nataka tu yale maneno yake yaingie kwenye *hansard* kwa lile aliloniahidi kwamba yale ambayo niliyoyazungumza kwa kufanya kikao na Mhe. Waziri wa Ardhi Sharif Ramadhan Abdalla Shaaban, ili kuweza kutatua yale matatizo. Ninafikiri akishanijibu hivyo tu, ikishaingia kwenye *hansard* Mhe. Mwenyekiti, leo nitakuwa sina tena buti. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Mwenyekiti, nataka nimuhakikishie tu Mhe. Hamza Hassan Juma kwamba leo nimekutana na Mhe. Waziri mwenzangu; Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban, tumekubaliana kikao kifanyike siku ya Jumatatu, saa tatu kamili asubuhi ofisini kwa Mhe. Ramadhan. Tumekubaliana wataalam wetu watakuwepo na tayari nimeshamjulisha Mhe. Hamza juu ya kukutana siku ya Jumatatu. Ahsante.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, unajua tatizo kanuni zetu mimi nilizungumza hapa kwenye hii *microphone* na *hansard* ikaingia na wewe ndio ulikuwa shahidi pale unasimamia, maana yake wewe ndio kama Jaji wetu. Kwa hivyo Mhe. Waziri kutokana na uswahibu wetu kaja kanifata, hayo aliyonambia keshanieleza, lakini

wewe shahidi wetu hukuyasikia. Sasa mwakani nikija nikimbana katika haya haya wewe itabidi ujiulize aa, alinijibu nini. Sasa nilikuwa nataka na wewe usikie hicho alichonijibu baadae tuendelee. Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Mhe. Spika: Ili niwe shahidi mzuri, hufanya nini huko katika mkutano.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, kulikuwa kuna tatizo la wawekezaji na wawekezaji wenyewe ni wazalendo, wamekuwa wanasumbuliwa sana na imefika pahala walikuwa wanataka kuwaiga wale wenzao waliohamia Tanzania Bara. Sasa Mhe. Waziri nikamueleza hiyo kadhia na akasema hili ni suala ambalo linahitaji tukae pande mbili; kuna watu wa ardhi na kuna wao watu wa Wizara ya Fedha kupitia ZIPA.

Sasa mimi naamini kwa hayo matatizo yalivyo mimi ninavyohisi wala sio matatizo ni mambo tu ya urasimu na kutokuelewana. Kwa hivyo ninaamini hicho kikao atakachokaa Mhe. Waziri wa Fedha na Mhe. Waziri wa Ardhi Sharif Ramadhan, pamoja na hao watendaji wao hata na mimi wakinishirikisha, wala si lazima kunishirikisha au wasinishirikishe. Mimi haja yangu wale wawekezaji wetu waweze kutatua yale matatizo yao, ili waweze kutoa ajira kwa wananchi wetu lakini vile vile waongeze uwekezaji katika nchi yetu. Ni hivyo tu.

Mhe. Spika: Ndio mnakubaliana Mhe. Waziri hayo.

Mhe. Waziri wa Fedha: Ndio tumekubaliana.

Kifungu 0401	Idara ya Mipango Sera na Utafiti	463,464,000
Kifungu 0701	Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali	3,279,417,000
Kifungu 0901	Idara ya Fedha za Nje	278,728,000
Kifungu 1301	Idara ya Uhakiki Mali na Mitaji ya Umma	535,558,000
Kifungu 1901	Idara ya Uendeshaji na Utumishi	3,621,502,000
Kifungu 2201	Idara ya Bajeti	9,272,572,000
Kifungu 2202	Chuo cha Uongozi wa Fedha	1,800,300,000
Kifungu 2203	Bodi ya Mapato Ofisi Kuu Zanzibar	8,300,000,000
Kifungu 2205	Mfuko wa Barabara	7,102,000,000
Kifungu 2206	Mamlaka ya Uwekezaji, Vitega Uchumi Zanzibar	250,000,000
	Jumla ya Fungu	**36,067,700,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

Kifungu 9101	Mfuko Mkuu wa Serikali	69,825,100,000
	Jumla ya Fungu	**69,825,100,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

Kifungu 0401	Idara ya Mipango Sera na Utafiti	35,737,501,000
Kifungu 0701	Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali	020,000,000
Kifungu 0901	Idara ya Fedha za Nje	2,739,000,000
Kifungu 1301	Idara ya Uhakiki Mali na Mitaji ya Umma	3,000,000,000
	Jumla ya Fungu	**41,496,501,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

(Baraza linarudia)

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha Makadirio ya Wizara ya Fedha bila ya mabadiliko, sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza liyakubali makadirio hayo. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Niwahoji Waheshimiwa Wajumbe, wale wanaokubaliana na Makadirio ya Wizara ya Fedha wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Kuna shughuli nyengine Katibu.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti nimeombwa kutoa utaratibu baada ya Ofisi yako kutuletea Gazeti Rasmi la Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuhusu miswada ambayo itasomwa mara ya kwanza pengine tunategemea siku ya kesho na baadae katika kikao cha mwezi wa kumi. Miswada hii itakuja kuwasilishwa rasmi.

Kutokana na uzoefu wangu hapa Barazani baada ya kuangalia tu kwa ghafla huu Mswada mmoja wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Wauguzi na Wakunga; nilikuwa nahisi mswada huu ni mzito, ninahisi kwamba Wizara ya Afya kabla ya mswada huu kuja kuletwa Barazani basi vizuri ingetolewa taaluma ya semina kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, wakaeleweshwa vizuri ili tusije tukapitisha kitu kikaja kikatuletea athari kwa jamii yetu.

Kwa bahati mbaya sana wananchi wetu hatuna utamaduni sana wa kuwapelekea hii miswada wakenda wakaipitia kifungu hadi kifungu. Sasa hilo lilikuwa ombi langu maalum, ingawa Mheshimiwa Waziri wa Afya sasa hivi hapa hayupo lakini ninajua Naibu wake yupo na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ambaye ndie kiongozi wa shughuli za serikali, kwa sababu tunahitaji kupitisha miswada ambayo itasaidia zaidi kuimarisha afya za wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kuweza kunivumilia. Ahsante.

Mhe. Spika: Hiyo haikuwa kwa utaratibu isipokuwa ilikuwa ni ombi. Ombi hilo ninafikiri Serikali imesikia na watalifanyia kazi.

Waheshimiwa Wajumbe nichukuwe nafasi kuwashukuru sana kwa mashirikiano makubwa. Hali yetu ilikuwa ni ngumu kidogo, lakini hatimaye mumemudu kupitisha Makadirio yote ambayo yalikuwa yamewasilishwa kwa Wizara mbali mbali na kwa hiyo sasa kuhusiana na suala zima la bajeti, tumebakiwa na kazi moja kubwa; kazi ya mswada wa matumizi ambayo kazi hiyo ninafikiri itafanyika kesho, itakuwa ndio kazi ya kwanza na kazi inayofuata baada ya hapo, najua kuna kazi ya Wizara ya Wizara ya Ustawi wa Jamii, Uwezeshaji, Wanawake na Watoto kuhusu siku ya mtoto na baada ya hapo nitamuomba sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais atumalizie shughuli yetu kwa kufunga mkutano.

Sasa niwaombe sana Waheshimiwa Wajumbe tuoneshe mfano ulio mzuri. Niliwahi kuarifiwa wakati fulani kwamba kuna mfano wa Wabunge waliopitisha baadhi ya mambo, mimi sina hakika lakini nilipewa taarifa tu bila hata kuwepo *quorum*. Nadhani tufuate mifano iliyo mizuri. Huo si mfano mzuri kama umetendeka kweli. Kwa hivyo niwaombe sana Waheshimiwa Wajumbe tuwahi katika vikao vyetu. Huu ni wajibu wetu na kama ni wajibu basi tunalazimika kufata taratibu kama tulivyojipangia.

Ninawashukuru sana kwa mashirikiano makubwa. Kwa kazi hii ya leo ambayo mumeimaliza, kazi ambayo imetusumbua kidogo wakati wa asubuhi lakini hatimaye kwa Baraka za Mwenyezi Mungu na mwezi Mtukufu wa Ramadhani unaokaribia, shughuli hii imefanyika kwa ufanisi mkubwa. Ninawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe.

Kwa kuwa hakuna kazi nyengine na muda haujafika tukubali tu kwamba tusitishe shughuli zetu hizi hadi kesho tarehe 28/06/2014 siku ya Jumamosi saa 3:00 barabara za asubuhi.

(Saa 12:46 Baraza liliahirishwa hadi tarehe 28/06/2014 Saa 3:00 asubuhi)